

## Maswali

1. Mungu aliambia Musa afanye nini ili apeleleze Nchi ya Ahadi?
2. Wapelelezi walitakiwa wachunguze nini?
3. Iliwachukuwa wapelelezi muda gani kuchunguza?
4. Wapelelezi walirudi na nini kutoka huko?
5. Wapelelezi walisema nini juu ya miji za huko?
6. Wapelelezi walisema nini juu ya watu wa huko?
7. Wapelelezi 10 walisema nini?
8. Nani aliamini Mungu na akasema atawasaidia kushinda nchi hiyo?
9. Watu walifanya nini?
10. Mungu waliwaadhibu watu namna gani kwa sababu hawakumwamini?

## Majibu

1. Mungu aliambia Musa atume wapelelezi 12 waende wazunguke wakichunguza hiyo nchi.
2. Walikuwa wachunguze juu ya matunda, miji na watu.
3. Iliwachukuwa siku 40 wakizunguka nchi wakiichunguza.
4. Walirudi na kifurushi kikubwa cha mizabibu kilichobebwa katikati ya watu wawili. Pia walileta tini na mikomamanga.
5. Miji zilikuwa kubwa na kuzungukwa na kuta za nguvu.
6. Watu walikuwa wa nguvu tena kulikuwa na majitu.
7. Wapelelezi 10 waliogopa wakisema hawataenda kupigana.
8. Yoshua na Kalebu waliamini Mungu.
9. Watu waliogopa. Hawakuamini Mungu. Waliamua kuchagua kiongozi mwingine na warudi Misri.
10. Mungu aliwafanya Waisraeli warande rande jangwani kwa miaka 40. Watu wote wenye hawakuamini Mungu walikufia jangwani.

# SHULE YA JUMAPILI YA CBM

Awamu ya 1 Mwaka wa 3



## 17 Wapelelezi 12 wanaenda kwa Nchi ya Ahadi

### Marejeo

Hesabu 13:1 – 3; 17 – 20; 23 – 24; 25 – 33

Hesabu 14:1 – 4; 26 – 34

### Kiini cha somo

Kuonyesha kwamba, kwa vile Waisraeli hawakuamini Mungu waliadhibiwa na hawakuungia kwa Nchi ya Ahadi

### Maneno maalum

- 17.1 Nchi ya Hadi + wapelelezi 12 + chunguza + watu + miji + matunda
- 17.2 Wapelelezi 12 + miji + kuta za nguvu + majitu + mizabibu kubwa
- 17.3 Siku 40 + wapelelezi walisema + matunda mazuri + miji ya nguvu + majitu
- 17.4 Wapelelezi 10 + ogopa + sahadu Mungu + watu wanaogopa
- 17.5 Wapelelezi 2 + Yoshua na Kalebu + hawakuogopa + amini Mungu
- 17.6 Adhabu + miaka 40 + jangwani + Yoshua na Kalebu + enda kwa Nchi ya Ahadi

**17.1** Mwishowe Musa na Waisraeli walifika karibu na Nchi ya Ahadi. Wote walifurahia sana. Muda si muda wataingia kwa nchi yenye waliahidiwa na Mungu. Mungu aliwambia kwamba ilikuwa nchi nzuri yenye chakula kingi kinakua vizuri. Waisraeli walitakiwa wapigane washinde ili waichukue na waishi.

Waisraeli walitakiwa wajue hiyo nchi ya ahadi na watu walioishi kule. Halafu wafanye mipango ya kuishambulia. Mungu angekuwa nao na kuwasaidia wapigane washinde na waishi kule.


Mungu alimwambia Musa achague mtu mmoja kutoka kwa kila kabila kumi na mbili ya Waisraeli. Musa alituma hawa watu kumi na wawili waende kwa Nchi ya Ahadi na wafanye upelelezi juu ya nchi na watu wanaoishi kule.

Musa aliwambia hao watu kumi na wawili wafanye nini hasa. Lazima waende wapeleleze hiyo nchi vizuri. Lazima wakwee mlima mmoja mrefu penye wanaweza kuona hiyo nchi vizuri. Lazima wachunguze kama wale watu wa kule ni wa nguvu au wanyonge, tena ni wengi au wachache. Lazima waangalie kama miji za huko ni kubwa au ndogo na kama zimezungukwa na kuta za nguvu. Lazima waangalie kama nchi hiyo ni nzuri kwa kukuza mimea na miti. Musa aliwambia wawe na ujasiri wakienda kupeleleza hiyo nchi.

**17.2** Wale wapelelezi 12 walisafiri nchi yote na kuona kila kitu walichotakiwa kuona. Waliona kwamba miji zingine zilikuwa mzee sana na zingine zilikuwa kubwa na kuta za nguvu zimezunguka. Watu wa huko walikuwa watu wa nguvu na kulikuwa na pahali pengine kulikuwa na majitu. Waliona kwamba nchi ilikuwa nzuri ya kupanda mimea. Kulikuwa na matunda mengi na mazuri sana.

Wapelelezi walitaka kuchukuwa vitu fulani ili wapeleke wawaonyeshe Waisraeili. Walitelemka mpaka kwa mto na wakapata vifungu kubwa vya mizabibu. Walikata kifungu kimoja. Kilikuwa kubwa na mzito mpaka ikawabidi wakate kijiti, waifunge katikati ili wabebe watu wawili. Wapelelezi wengine walibeba tini na mikomamanga.

**17.3** Wapelelezi walikaa kule kwa muda mrefu. Iliwachukua siku arobaini kuchunguza hiyo nchi. Lakini baadaye walirudi. Watu wote wa Israeli walikuja kusikia habari ya wapelelezi. Walisema kwamba Nchi ya Ahadi ilikuwa nchi nzuri sana. Kulikuwa na mimea mizuzi na matunda mengi. Waliwaonyesha matunda mazuri yaliyoletwa kutoka kwa hiyo nchi – kifungu kikubwa cha mizabibu, tini na mikomamanga. Wapelelezi walisema kwamba kulikuwa na miji mikubwa na zilikuwa na kuta za nguvu zilizunguka, tena watu wa huko walikuwa watu wa nguvu. Pia waliona majitu kwa hiyo nchi.



**17.4** Wapelelezi 10 walisema kwamba waliogopa kwenda kupigana na kuchukua nchi kwa sababu ya wale watu wa nguvu, majitu na kuta za nguvu zilozunguka miji. Walikuwa wamesahahu ulinzi wa waajabu wa Mungu na miujiza alizofanya Misri. Tena walisahahu Mungu. Waliwasikiliza wapelelezi kumi na wakaogopa. Walitamani kama wangebaki Misri. Tena walitaka kuchagua kiongozi mpya ili awarudishe Misri.

**17.5** Wapelelezi wawili, Yoshua na Kalebu, waliamini Mungu. Waliambia Waisraeli kwamba wasiogope kwa sababu Mungu atawasaidia. Lakini watu hawakusikiliza. Mungu hakupendezwa nao kwa sababu hawakumwamini.

**17.6** Mungu alisema kwamba Waisraeli watarudi nyuma watange tange jangwani mpaka wafe kama adhabu kwa sababu hawakumwamini. Waisraeli walitanga tanga jangwani kwa miaka arobaini. Watoto wao walikua na wakawa na ujasiri na imani kuu kwa Mungu kuliko wazazi wao. Walienda kwa Nchi ya Ahadi na Yoshua na Kalebu waliokuwa wameamini Mungu.